

TANGAZO LA SERIKALI NA. 406 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(2))(g) na (j)

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA ULINZI WA MIZIGO NA USALAMA WA
SHUGHULI ZA KIBANDARI ZA MWAKA 2024

- Jina
TS. Na.
387 la 2023
1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama wa Shughuli za Kibandari za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama wa Shughuli za Kibandari za Mwaka 2023 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni kuu”.
- Marekebisho ya kifungu wezeshi
2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kifungu wezeshi na badala yake kuweka kifuatacho:
“(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(2))(g) na (j)”
- Marekebisho ya kanuni ya 3
3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati ufuatao, kwa kuzingatia mtiririko wa alfabeti:
“mamlaka husika” maana yake ni Waziri, idara ya Serikali au mamlaka yenye mamlaka ya kutunga kanuni, amri au maelekezo mengine yenye nguvu ya sheria;
- Marekebisho ya kanuni ya 5
4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5-
(a) katika kanuni ndogo ya (1), kwa kufuta maneno “bila kujali” na badala yake kuweka maneno “bila kuathiri”; na
(b) katika kanuni ndogo ya (2) kwa-
(i) kufuta kivuo; na

(ii) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya
(2) kanuni ifuatayo:

“(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii
“sababu za msingi na zilizoainishwa”
zitajumuisha kutozingatiwa kwa sheria
husika, kanuni na maelekezo.”

Marekebisho
ya kanuni ya
12

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
12(a) kwa kufuta neno “hauwezi” na badala yake kuweka
neno “kuweza”.

Marekebisho
ya kanuni ya
14

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
14(4) kwa kuweka maneno “na behewa” katikati ya
maneno “lori” na “na”.

Marekebisho
ya kanuni ya
20

7. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
20(1):
(a) katika aya ya (c) kwa kufuta alama ya nukta
mkato pamoja na neno “na” kuweka alama na
badala yake nukta; na
(b) kufuta aya ya (d).

Marekebisho
ya kanuni ya
23

8. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
23 kwa-
(a) kuongeza kivuo mara baada ya kanuni ndogo
ya (1)(b) kama ifuatavyo:
“Isipokuwa kwamba, mwendesha
bandari au bandari kavu atahakikisha kuwa
vifaa au mifumo mbadala ya kupambana na
moto inakuwepo wakati wa zoezi la
majaribio au ukarabati na matengenezo”;
(b) kufuta maneno “zimewekwa wazi” yaliyopo
katika kanuni ndogo ya (4) na badala yake
kuweka maneno “zinafikika na ziko tayari kwa
kutumika”.

Marekebisho
ya kanuni ya
30

9. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
30 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2)
kanuni ndogo ifuatayo :

“(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, “mtu mwenye uwezo” maana yake ni mtu ambaye-

- (a) ana cheti husika kutoka katika taasisi ya mafunzo inayotambulika;
- (b) ana uzoefu wa angalau mwaka mmoja wa uendeshaji wa mitambo ya kunyanyulia vyombo na zana; na
- (c) ameidhinishwa na mamlaka husika.”.

Marekebisho ya kanuni ya 34

10. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 34 kwa kufuta maneno “bila kujali” na badala yake kuweka maneno “bila kuathiri”.

Marekebisho ya kanuni ya 53

11. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 53(2) kwa kuweka maneno “kuhusiana na ulinzi na usalama” katikati ya maneno “mafunzo” na “ya”.

Marekebisho ya kanuni ya 55

12. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 55(3) kwa kuongeza maneno “awali ya” katikati ya maneno “ya” na “uchunguzi”.

Marekebisho ya kanuni ya 57

13. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 57 kwa kufuta maneno “mbili”, “ishirini” na “mwaka mmoja” na badala yake kuweka maneno “ishirini”, “arobaini” na “miaka miwili,” “mtawalia.”

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

14. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa:

- (a) kufuta tarakimu “5” inayoonekana katika kifungu wezeshi cha Fomu Na. 1 na badala yake kuweka tarakimu “5(1)”; na
- (b) kufuta tarakimu “8(1)” inayoonekana katika kifungu wezeshi cha Fomu Na. 2 na badala yake kuweka tarakimu “8(2)”.

*Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ulinzi wa Mizigo Na Usalama wa Shughuli
za Kibandari*

Tangazo La Serikali Na. 406 (Linaendelea)

Marekebisho
ya Jedwali la
Pili

15. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la
Pili kwa kufuta tarakimu “52(1)” inayoonekana katika
kifungu wezeshi na badala yake kuweka tarakimu
“51(2)”.

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Uchukuzi